# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE EIGHT: “Life in a Bubble”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI:Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: LINDA AND FLORENCE IN A FAST FOOD RESTAURANT**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **MR. MARAGA**

**SCENE TWO: FARAHANI AND SULE WALKING ON THE BEACH**

- **Farahani (m, 19)**
- **Sule (m, 19)**

**SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE AT A NIGHTCLUB**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Client (m, 40)**
- **Sandra (f, 30)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika makala nyingine ya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hii ni sehemu ya nane kwenye mfululizo wa mchezo huu **“Ardhi ya Ahadi, kuhusu Waafrika Wanaohamia Ulaya.”** Katika kipindi kilichotangulia, Linda ananunuliwa zawadi na rafiki yake Florence, ambaye ameanza kushuku ukarimu wake. Yaonekana kuna njama! Nyumbani Afrika, Wazazi wa Linda wamefutwa kazi. Mzee Maraga ameghadhabika sana asijue la kufanya, hadi pale mkewe anapomfahamisha kwamba Linda anaweza kuwasaidia kifedha akiwa Ulaya. Ama kwa hakika, Linda na wazazi wake wanaonekana kuishi maisha tofauti.- Wote wanajaribu kuhifadhi siri zao. Je! ni nini kitakachojiri wakati mambo yanapozidi kupamba moto? Hebu tusikie kwenye kipindi hiki cha leo **“Maisha kama Povu”.** Na moja kwa moja, tunaungana na Linda na Florence kwenye mgahawa wakila chakula.

## SCENE ONE: LINDA AND FLORENCE AT A FAST FOOD RESTAURANT

1. **SFX: FAST FOOD RESTAURANT ATMO**

2. **FLORENCE:** Kama unataka kufaulu huku Ulaya ukiwa mhamiaji, kwanza lazima upate vibali vyote vya uhamiaji. Na watu hutumia njia tofauti tofauti.

3. **LINDA:** **(curious)** Kujihalalisha? Mbona siikuelewi. Nilikuja Ulaya kihalali na viza ya mwanafunzi! Kwa kweli nisingeruhusiwa kusoma hapa kama mhamiaji asiye halali.

4. **FLORENCE:** **(loud whisper)** Sshh! Usizungumze kwa sauti ya juu Linda. Nafahamu vyema kwamba umekuja Ulaya kwa viza ya mwanafunzi. Lakini bado kuna vikwazo vingi sana kwa wanafunzi wa kigeni kufanya kile wanachotaka. Namaanisha kupata uraia! Unahitaji kibali cha kufanya kazi. Na hadi pale utakapopata kibali cha kufanya kazi ndipo utaanza kuishi maisha mazuri kama mimi.

5. **LINDA:** Sawa. Naelewa sasa. Na unanishauri nifanye nini?

6. **FLORENCE:** Kupitia ndoa.

7. **LINDA:** Una maana kuolewa? Sasa kuolewa na Chivasi kutasaidia vipi kuishi maisha bora hapa Ulaya?

Bado sikuelewi!

**8. FLORENCE:** **(laughs out)** Chivasi!? Hahaha! Kumbe wewe bado mshamba sana! Kuanzia sasa sahau kabisa mambo ya Chivasi! Wewe mwenyewe umesema-hayupo tena katika maisha yako hapa Ulaya. Lazima uolewe na Mzungu!

**9. LINDA:** **(shocked)** Nini? Hapana! Florence, unawezaje kunishauri hivyo? Ni kweli huenda niko mbali na Chivasi na kwa muda mrefu, na tayari nafahamu nimemdanganya kuhusu maisha yangu huku, lakini bado nampenda!

**10. FLORENCE:** Subiri kwanza …! Ni sawa unaweza kuendelea kumpenda. Hilo si tatizo. Naweza kufanya mipango ukaolewa kisiri. Na si lazima ukutane naye kabla ya harusi. Na pia si lazima umfahamu kimapenzi. Ila tu kwa kujifanya nyinyi ni wanandoa. Na baada ya muda mfupi utapata vibali vyote pamoja na hati ya kufanya kazi Ulaya.

**11. LINDA:** Hilo tu? Mbona sikuamini! Kwa lengo gani hasa? Kwanza uliniambia niwe na subira na pia kujitolea. Sasa nitasubiri hadi lini? na kujitolea kivipi?

**12. FLORENCE:** **(thoughtful)** Hmm… ni kweli. Kuna faida yake! Na si jambo gumu. Unahitajika kumlipa mume wako bandia.

**13. LINDA:** Nimlipe? Nilidhani wanaume ndio wanaotoa mahari kwa wachumba wao? Na ni wapi nitapata pesa hizo ikiwa sina kazi?

**14. FLORENCE:** Usijali. Ukiamua kwa dhati ya moyo wako, vinginevyo si tatizo! Utamlipa kwa njia ya pole pole kila mwezi kuanzia siku ya kufunga ndoa hadi pale utakapopata stakabadhi zako. Lakini katika kipindi hicho lazima uwe na subira sana. Ni rahisi!

**15. LINDA:** **(thoughtful)** Kwa hivyo, ina maana kuwa itakuwa nimepata vyeti vya ndoa lakini kwa njia isiyo halali. Sivyo?

**16. FLORENCE:** Hasa.

**17. LINDA:** Lakini Flo, je huyo mwanamume akitaka zaidi ya hizo pesa? Nitafanyaje? Kisheria tutakuwa tumeoana.

**18. FLORENCE:** Hawezi kufanya hivyo. Hana haki! Na ikiwa atafanya hivyo basi itategemea kauli yako. Watu wengine wamepitia njia hii na hatimaye kuishia kuwa wapenzi. Hilo lawezekana.

**19. LINDA:** **(scared)** Siwezi! Hapana sio mimi. Hapa nimekuja kusoma! Na ikiwa nitaamua kuolewa basi si kwa sababu nyingine ila hiyo tu ya kutaka kupata pesa na kuishi maisha mazuri.

**20. FLORENCE:** Vyema kabisa. Kwa hivyo umekubali? Uko tayari kufanya hivyo?

**21. LINDA:** Bado sijaamua, Flo! Huu ni uamuzi mgumu sana! Unafahamu kwamba unazungumzia suala la ndoa. Si jambo rahisi...! Nahitaji muda kulifikiria.

**22. FLORENCE:** Sawa. Lakini kumbuka kuna wasichana wengine huko nyumbani wanaotamani kupata nafasi kama hii.

**23. SFX: MOBILE PHONE RINGING**

**24. FLORENCE:** Ohh – samahani ni simu kutoka nyumbani. Halo, ni Florence hapa?

**25. MR. MARAGA:** Hello – samahani kwa kukusumbua. Mimi ni Babake Linda. Linda alinipigia simu kwa kutumia simu hii siku ya kwanza alipowasili Ulaya, na nafikiri kuwa nyinyi ni marafiki. Pengine unaweza kumpitishia ujumbe huu?

**26. FLORENCE:** Una bahati sana. Linda yuko hapa na mimi. Subiri kidogo nikupe Linda - Linda, ni Babako! Anataka

kuzungumza na wewe.

**27. LINDA:** **(nervous)** Baba, mko salama huko nyumbani?

**28. MR. MARAGA:** **(takes deep breath)** Tuko salama Linda. Hatuna neno!

**29. LINDA:** Vyema. Nimeshtuka, nikidhani pengine kumetokea matatizo. Haya nieleza ulichotaka kuniambia?

**30. MR. MARAGA:** Linda, sitaki uwe na hofu, lakini mimi na mamako tume…… tumefukuzwa kazi! Tafadhali usiwe na wasi wasi nilitaka tu kukufahamisha lakini tunajaribu kukabiliana na hali hiyo.

**31. LINDA:** **(shocked)** Oh poleni sana! Lazima mnapitia wakati mgumu sana?

**32. MR. MARAGA:** **(sadly)** Hatuna neno….tuko sawa. Usiwe na wasi wasi. Muda wangu wa maongezi umekwisha. Sitaweza kuzungumza nawe kwa muda mrefu.

**33. SFX: TELEPHONE CONNECTION DISCONNECTED ABRUPTLY**

**34. LINDA:** Baba! Baba! Hallo…? Baba bado uko…? – Amekata simu.

**35. FLORENCE:** Linda, kuna tatizo nyumbani?

**36. LINDA:** **(emphatically)** Tafadhali nitafutie kazi Florence. Kisha haraka sana! Kisha nitafutie mume wa Kizungu.

**37. NARRATOR:** Habari za kuachishwa kazi kwa wazazi wake kunamfanya Linda kufanya uamuzi wa haraka kuhusu anachotaka kufanya. Anafahamu vyema kwamba ndiyo njia pekee baada ya kumsikiliza babake akijaribu kuonesha ujasiri. Habari hizo zinamuacha Linda akitapatapa. Je! Florence anampangia nini Linda? Endelea kuwa nasi. Wakati huo huo, huko Afrika Kaskazini maandamano ya kisiasa yamepamba moto, na kugeuka ghasia za kikabila ambazo zimewaacha wengi bila makao na kutafuta hifadhi katika kambi za wakimbizi. Farahani na Sule ni miongoni mwa wale waliojikuta katikati ya ghasia hizo ambazo sasa zinachangia kuzorota kwa urafiki baina yao.

**SCENE TWO: FARAHANI AND SULE WALKING ON THE BEACH**

**38. SFX: OCEAN WAVES HITTING HARD ON SHORE**

**39. SULE:** Farahani, hata bahari pia imechafuka, sio kama tunavyoifahamu. Nahofia sana familia yangu, nchi yangu na sisi pia! Naona tutoroke sasa kabla mambo hayajachafuka zaidi.

**40. FARAHANI:** Tutorokee wapi?

**41. SULE:** Kwenda wapi? Mahali popote tu lakini sio kubaki hapa. Watu wengi wametorokea nchi jirani.

**42. FARAHANI:** Nchi jirani? Sule, sisi tumezoea ghasia hizi, ni jambo la kawaida mbona. Yanayoendelea kwa hakika si mazuri na yatazidi kuwa mabaya. Unajuaje ghasia hizi hazitasambaa hadi nchi hizo za jirani? Hii ndio fursa nzuri ya kuhamia Ulaya.

**43. SULE:** **(irritated)** Farahani! Wacha mzaha! Sahau ndoto yako hiyo ya kuishi Ulaya. Nchi yetu imetumbukia katika ghasia za kikabila, na jambo unalofikiria ni kuhamia Ulaya? Ndio Afrika si mahali pazuri pa kuishi lakini hapa ndiyo nyumbani. Muhimu ni kuonesha uzalendo.

**44. FARAHANI:** **(angry)** Usijaribu tena kunikumbusha kuhusu majukumu yangu ya uzalendo! Ukiwa unataka kuhamia nchi nyingine ya Kiafrika, basi mimi simo, niache tu nifuate shughuli zangu Sule, umenielewa? Niache na mambo yangu!

**45. SULE:** **(furious)** Niachane na wewe? Sawa nitaachana na wewe kabisa. Na pengine ningekuwa nimefanya hivi mapema sana. Hata hivyo lakini.... kawia ufike. Nakutakia kila la kheri na ndoto yako ya Ulaya Farahani. Farahani!

**46. SFX: FAST WALKING ON SAND**

**47. FARAHANI:** **(calling after him)** Sule! Sule, Samahani sana. Hebu nisubiri! Kumbuka sisi ni ndugu?

**48. SULE:** **(from afar)** Ndugu hufa pamoja. Wewe una ubinafsi mwingi sana!

**49. FARAHANI:** **(shouting)** Sule! Sule!

**50. SFX: OCEAN WAVES HIT HARDER AND LOUDER ON SHORE**

**51. NARRATOR:** Farahani anaitazama bahari kuelekeza macho yake Ulaya. Lazima sasa afanye uamuzi: kudumisha urafiki au kutimiza ndoto yake ya kuhamia Ulaya. Je! ni upi utakuwa uamuzi wake? Endelea kusikiliza … Wakati huo huo, bila ya kupoteza wakati Florence amemtafutia kazi Linda, ambaye anahitaji pesa kwa haraka sana sio tu kujikimu kwa mahitaji yake bali pia kuisaidia familia yake. Tuungane na Linda katika siku yake ya kwanza kazini, anakokaribishwa na Sandra. Mwafrika ambaye pia amehamia Ulaya.

**<u>SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE AT A NIGHTCLUB</u>**

**52. SFX: EUROPEAN NIGHTCLUB ATMO - LOUD TECHNO MUSIC**

**53. FLORENCE:** **(trying to speak loudly)** Kwa hiyo Linda, mambo yameanza kukunyokea. Hapa ndipo utakapofanya kazi. Utakuwa ukiwahudumia wateja hapa. Si ni kazi rahisi. Ukiwa na swali muulize Sandra hapa. Amekuwa akifanya kazi hapa kwa zaidi ya miaka mitatu sasa. Nakutakia kila la kheri!

**54.** **LINDA:** **(uncertain)** Lakini… hapa ni…

**55.** **SANDRA:** Habari, naitwa Sandra- Usijali utazoea tu! Kufanya kazi usiku huwa ngumu siku za kwanza, lakini ukizoea utafurahia pesa utakazokuwa ukipata. Kwanza bakshishi!

**56.** **LINDA:** **(still doubtful)** Habari Sandra, Naitwa Linda. Sasa nitafanya kazi hadi saa ngapi usiku. Mimi ni mwanafunzi wa chuo kikuu, na lazima pia niende chuoni kesho!

**57.** **SANDRA:** Hapa tunafanya kazi hadi mteja wa mwisho atakapoondoka. Leo ni mwisho wa wiki na kutakuwa na shughuli nyingi sana. Nadhani tunaweza kufanya kazi hadi asubuhi.

**58.** **LINDA:** Na malipo je? Unalipwa pesa ngapi?

**59.** **SANDRA:** Inategemea! Sistahili kukueleza haya, Kwani mimi pia nafanya kazi hapa kinyume na sheria. Sina vibali vya kufanyia kazi, hivyo huwa nategemea bakshishi tu kutoka kwa wateja! Mshahara ni midogo sana, na mara nyingine hata hatulipwi kabisa. Lakini tufanye kazi! Kuna mteja pale anasubiri. Nenda ukamuhudumie.

**60. SFX: LINDA WALKING ACROSS THE CLUB - MUSIC SWELLS AND FADES - LAUGHTER AND VOICES**

**61. LINDA:** Habari za jioni, nikuletee nini?

**62. CLIENT:** **(flirtatiously)** Oh! tuko na mgeni! Kisha mrembo sana! Hebu njoo hapa…. ! Mm mrembo kweli...! Hebu songa karibu nami.. .hasaa....

**63. LINDA:** **(screaming)** Hapana hebu usinishike!

**64. SFX: BOTTLE FALLS TO FLOOR AND BREAKS**

**65. CLIENT:** **(laughing)** Hahaha!… nimekupenda,,! sura yako inavutia na tabia pia…shika pesa uniletee pombe, na chenji uchukue kama bakshishi!

**66. SANDRA:** **(furious)** Linda! Unafanya nini? Unataka kufukuza wateja?

**67. LINDA:** **(trembling)** Sandra, huoni anafanya nini? Siwezi kukubali tabia hizi zake! Na kama hii ndio kazi wacha ikae!

**68. SANDRA:** Linda, nilikwambia siku za kwanza kawaida huwa ngumu. Lakini kumbuka siku zote mteja ndiye mwenye haki. Kwani amekuagiza kinywaji gani?

**69. LINDA:** Pombe. Amenipa euro 20 na akaniambia nichukue chenji .

**70. SANDRA:** **(enthusiastic)** Unaona sasa! Una bahati sana msichana. Ni siku yako ya kwanza kazini na umepata Bakshishi kubwa kiasi hicho! Nenda umletee kinywaji! Ukiendelea hivi, usiku mmoja unaweza kupata pesa nyingi zaidi ya mshahara wako wa mwezi.

**71. LINDA:** Sandra, Ni nikuulize?

**72. SANDRA:** Nini tena? Hapa tuko kazini, Linda. Huku Ulaya watu hufanya kazi kama mchwa. Hawataki upoteze hata dakika moja. Sawa. Unataka kujua nini?

**73. LINDA:** Nani mwenye hii klabu?

**74. SANDRA:** Unataka kujua ndiyo iweje? Hilo si muhimu kwa sasa. Twendelee na kazi!

**OUTRO:**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa sehemu hii ya nane kwenye mfullizo wa mchezo huu “**Ardhi ya Ahadi- hadithi kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya.**” Je unadhani maisha yatambadilikia Linda baada ya kupata kazi? Na je atakubali kuendelea na mipango yake ya kutafuta cheti bandia cha ndoa ili kupata uraia au atabadili nia baada ya kupata kazi? Na Florence naye

anafaidika kivipi kwa kumsaidia Linda? Je! huu ndio mwisho wa urafiki baina ya Farahani na Sule? Usikose kuungana nasi katika kipindi kinachofuata. Pia ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea ukurasa wetu wa dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.